Middle Ear Infection (Swahili)

# Maambukizi ya sikio la kati



Maambukizi ya sikio la kati (pia huitwa acute otitis media) ni maambukizi nyuma ya kiwambo cha sikio.

Maambukizi haya ni ya kawaida sana kwa watoto wadogo kwa sababu wana mirija midogo (inayoitwa Eustachian tubes) inayounganisha sikio la kati na koo.

Watoto wanapopata mafua, vijidudu kutoka koo vinaweza kusafiri hadi sikio la kati na kusababisha maambukizi.

## Ishara na dalili

- Maumivu ya sikio
- Kuvuta au kusugua sikio hasa wakati wa kulala chini (watoto wachanga na watoto wadogo)
- Kukasirika (kuhisi hasira na kuudhika), kulia sana
- Homa (halijoto juu zaidi ya 38°C)
- Pua yenye makamasi mengi, koo ya kuumia au kikohozi
- Majimaji au damu inayotoka sikioni (hii ni ishara ya kiwambo cha sikio kilichopasuka).

## Matibabu

Paracetamol (Panadol au Dymadon) na Ibuprofen (Nurofen) kwa kawaida ni tiba pekee ya maambukizi ya sikio la kati. Fuata maelekezo kwenye chupa au paketi kwa kipimo cha sahihi. Usimpe mtoto wako kipimo zaidi ya kile kinachopendekezwa kwa siku. Maumivu kutoka kwa maambukizi ya sikio la kati kawaida huisha ndani ya siku moja hadi mbili hata bila matibabu.

Ikiwa mtoto wako bado ana maumivu baada ya saa 48, daktari wako anaweza kukupa dawa kali zaidi ya maumivu au viua vijasumu kutibu maambukizi. Viua vijasumu na dawa za ya mvilio hazitasaidia mtoto wako.

## Utunzaji wa nyumbani

Mpe mtoto wako dawa ya kupunguza maumivu, inapohitajika. Fuata maelekezo kwenye chupa au paketi kwa kiasi kilichopendekezwa cha dawa ili kumpa mtoto wako. Usimpe zaidi kuliko kiasi kilichopendekezwa kwa siku.

Ikiwa mtoto wako ana kiwambo cha sikio kilichopasuka, haipaswi kupata maji yoyote katika sikio lake kwa angalau siku 10 au mpaka ipone. Daktari wako ata hitaji kuangalia sikio la mtoto wako ili kuhakikisha limepona.

Tembelea daktari ya mtoto wako mara tu anapomaliza dawa zake za viuavijasumu ili kuhakikisha kuwa maambukizi yameondoka.

Watoto huwa salama kusafiri kwa ndege wiki 2 baada ya maumivu yameondoka.

## Wakati wa kuonana na daktari

Mwona GP wako ikiwa mtoto wako:

- ana ishara na dalili za maambukizi ya sikio la kati na ana umri wa chini ya miezi 6
- ana dalili kwa zaidi ya siku 2
- ana dalili ambazo zinakuwa mbaya zaidi
- ana uvimbe na unyekundu nyuma ya sikio
- ana umajimaji unaotoka sikioni
- ni mtu wa Asili au wa Visiwa vya Torres Strait (kwa sababu ana hatari kubwa ya kupata maambukizi)
- anasafiri kwa ndege wiki 1 baada ya kupata maambukizi.

Daktari wako ataangalia ndani ya sikio la mtoto wako kwa kutumia kifaa maalum chenye lenzi ya kukuza na tochi ili kusaidia kutambua maambukizi.

Mtoto wako anapaswa kumuona daktari wake miezi 3 baada ya kuambukizwa ili kuhakikisha kuwa majimaji yote yaliyo nyuma ya kiwambo cha sikio yametoka.

Ikiwa mtoto wako ana maambukizi mengi ya sikio, unapaswa kupimwa kusikia kwake na mtaalamu wa kusikia (audiologist).

Daktari wako anaweza pia kumwelekeza kuonana na daktari wa watoto au mtaalamu wa masikio, pua na koo (ENT).

Imeandaliwa na Idara za Dharura na Upasuaji wa Kichwa na Shingo, Hospitali ya Watoto ya Queensland.
Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi. **Resource ID**: FS166 **Reviewed**: July 2022

**Kanusho:** Maelezo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husasishwa kila mara, kwa hivyo tafadhali angalia kuwa unarejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.